



MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI AFRIKA MASHARIKI (EACOP)

TAARIFA YA MAPOKEZI YA CHETI CHA ITHIBATI YA TATHMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA

DODOMA, TANZANIA

06 FEBRUARI 2020

Total East Africa Midstream B.V. (TEAM B.V) kampuni inayosimamia Mradi¹ wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)² umepokea Cheti cha Ithibati ya Tathmini ya Mazingira kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mradi wa EACOP nchini Tanzania: Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki katika nchi kavu lenye urefu wa kilometa 1147, Kituo cha Kuhifadhi Mafuta pembezoni mwa bahari, Gati iliyo katika bahari na Kituo cha Kupakia Mafuta .

Lengo la Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki ni kusafirisha mafuta yanatopatikana Uganda katika vitalu vilivyo pembezoni mwa ziwa Albert.

Nchini Tanzania shughuli za Mradi za kujenga na kusimamia bomba refu zaidi duniani la kusafirisha mafuta ghafi linalopashwa joto kwa njia ya umeme zitafanyika katika mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga.

Tathmini ya Athari za Kimazingira ilifanyika katika kipindi cha mwaka 2017 na 2018 ikitathmini maswala ya kimazingira na kijamii kwa kushirikisha kwa ukaribu wadau wote.

Ripoti ya kwanza iliwasilishwa katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) tarehe 21 Desemba 2018. Baada ya kupitiwa kwa kina, kushirikisha viongozi wa mikoa na wilaya, jamii na makundi husika, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), ripoti ya mwisho baada ya kufanyia kazi maoni ya Baraza iliwasilishwa kwa Baraza na Cheti cha Ithibati ya Tathmini ya Athari za Kimazingira kilitolewa tarehe 21 Novemba 2019.

¹ Huu ni Mradi unaoendeshwa na sekta binafsi kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania na Uganda.

² Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki linaundwa na bomba la inchi 24 linalotunza joto na kufukiwa ardhini, vituo sita vya kusukuma mafuta (viwili viko nchini Uganda na vinne viko Tanzania), vituo viwili vya kupunguza kasi ya mafuta vyote viko nchini Tanzania pamoja na Kituo kwa ajili ya usafirishaji wa mafuta kilicho katika eneo la bahari. Mafuta ya Uganda yana asili ya uzito na hali ya nta hivyo kuhitaji mafuta hayo kusafirishwa katika kiwango cha nyuzi joto 50° ili yaweze kufikia kiwango cha kutiririka. Ili kuhakikisha bomba linakuwa na kiwango cha joto kinachohitajika, bomba litapashwa joto kwa njia ya umeme, na kulifanya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kuwa bomba refu zaidi duniani linalopashwa joto kwa njia ya umeme.



Shughuli za makabidhiano ya Cheti cha Ithibati imefanyika katika ofisi ya Makamu wa Rais mkoani Dodoma na imeshuhudiwa na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira Mheshimiwa Mussa Hassan Zungu. Pia imeshuhudiwa na watendaji kutoka katika Baraza, Wizara ya Nishati na Kitengo cha Mazingira cha Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kampuni ya TEAM B.V inashirikiana kwa ukaribu na Serikali ya Tanzania na inategemea kuendelea kufanya kazi pamoja na Serikali ili kutekeleza Mradi mara makubaliano ya Kisheria na Kibiashara yatakapokamilika.

Bomba la Mafuta Ghafi litafungua fursa Afrika Mashariki kwa kuvutia wawekezaji. Mradi utapelekea ongezeko la Fedha za moja kwa moja za Kigeni (FDI) nchini Uganda na Tanzania katika kipindi cha ujenzi.

-MWISHO-

Kwa taarifa zaidi au kufanya mahojiano kwa ajili ya vyombo vya habari tafadhali wasiliana nasi kupitia:

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano,

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi - Tanzania

Mariagoreth Charles,

Ofisi: +255 22 2214100/4102/4103 **Simu ya Mkononi:** +255 699 000 341

Barua Pepe: mariagoreth.muangirwa@external.total.com

Tovuti: www.eacop.com